**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA**

**UPIMAJI WA KITAIFA WA DARASA LA NNE**

**03** **HISABATI**

**Muda: Saa 1: 30** **Mwaka: 2022**.

**Maelekezo**

1. Mtihani huu una jumla ya maswali **matano (5)**
2. Jibu maswali **yote**

Katika swali la 1 – 5, kokotoa swali ulilopewa na kisha andika jibu sahihi kwenye nafasi iliyotolewa.

| Na. | | Swali | Sehemu ya Kazi | Jibu |
|---|---|---|---|---|
| **1.** | a) | Ana alipewa chungwa, akala $\frac{1}{4}$ ya chungwa hilo. Ni sehemu gani iliyobaki? | | |
| | b) | Andika 99,001 kwa kirefu | | |
| | c) | Thamani ya namba X katika namba XVIII ni | | |



Find this and other free resources at:
https://maktaba.tetea.org

| Na. | | Swali | Sehemu ya Kazi | Jibu |
|---|---|---|---|---|
| | d) | Andika kwa kirumi namba iliyopo kati ya 48 na 50 | | |
| | e) | Ni namba gani itajumlishwa na 4,392 ili kupata 7,005? | | |
| **2.** | a) | Hatua moja ya kobe ni sm 5. Je, atatembea hatua ngapi kufikia sm 30? | | |
| | b) | Juliasi ana watoto watano wanaopishana umri kwa miaka 5 kila mmoja. Ikiwa mtoto wa kwanza ana miaka 35, je mtoto wa nne ana umri gani? | | |
| | c) | Nchi nne zilipata uhuru wao kama ifuatavyo: Kenya 1962, Tanganyika 1961, Uganda 1963 na Zimbabwe 1980. Je, ni nchi ipi ilikuwa ya kwanza kupata uhuru? | | |
| | d) | Matokeo ya Gladness ya majaribio ya mwezi yaliongezeka kwa alama 12 kila mwezi. Ikiwa mwezi wa kwanza alipata alama 186, je, mwezi wa nne alipata alama ngapi? | | |





Find this and other free resources at:
https://maktaba.tetea.org

| Na. | | Swali | Sehemu ya Kazi | Jibu |
|---|---|---|---|---|
| | e) | Shule ya msingi Mji mpya huchagua viongozi wake kila baada ya miaka 2. Ikiwa uchaguzi wa mwisho ulifanyika mwaka 2018, uchaguzi unaofuata ulifanyika mwaka gani? | | |
| **3.** | a) | Tafuta tofauti ya 39,365 na 33,868 | | |
| | b) | Aisha amegawanya maembe 350 katika mafungu 10 yenye idadi sawa. Je, kila fungu lina maembe mangapi? | | |
| | c) | Baraka hulipwa shilingi 4,000 kwa siku. Ikiwa anafanya kazi kwa siku 40, jumla atalipwa shilingi ngapi? | | |
| | d) | Joel alinunua redio na kuiuza kwa shiingi 60,500. Ikiwa alipata faida ya shilingi 20,000, je, aliinunua redio hiyo kwa shilingi ngapi. | | |
| | e) | Kuku huatamia mayai kwa muda wa siku 21. Je, muda huo ni sawa na majuma mangapi? | | |



Find this and other free resources at:
https://maktaba.tetea.org

<table>
<tr><th colspan="2">Na.</th><th>Swali</th><th>Sehemu ya Kazi</th><th>Jibu</th></tr>
<tr><td>4.</td><td>a)</td><td>Panga vipimo vifuatavyo kuanzia kikubwa hadi kidogo: m 900, sm 2, km 3 na mm 400</td><td></td><td></td></tr>
<tr><td></td><td>b)</td><td>Kipi ni kirefu zaidi kati ya waya wa sentimeta 20 na uzi wa meta 2?</td><td></td><td></td></tr>
<tr><td></td><td>c)</td><td>Kuna vipande vingapi vya mstari katika mstari ufuatao?<br><br></td><td></td><td></td></tr>
<tr><td></td><td>d)</td><td>Tafua mzingo wa pembetatu ifuatayo:<br><br></td><td></td><td></td></tr>
<tr><td></td><td>e)</td><td>Mzingo wa mraba n ism 196. Tafuta urefu wa upande mmoja</td><td></td><td></td></tr>
<tr><td>5.</td><td></td><td>Jedwali lifuatalo linaonesha idadi ya wanafunzi waliomaliza darasa la saba katika shule ya msingi Muungano kwa miaka mine:
<table>
<tr><th>Mwaka</th><th>Idadi ya Wanfunzi</th></tr>
<tr><td>2014</td><td>80</td></tr>
<tr><td>2015</td><td>90</td></tr>
<tr><td>2016</td><td>95</td></tr>
<tr><td>2017</td><td>98</td></tr>
</table></td><td></td><td></td></tr>
</table>



Find this and other free resources at:
https://maktaba.tetea.org

| Na. | | Swali | Sehemu ya Kazi | Jibu |
|---|---|---|---|---|
| | a) | Mwaka gani wanafunzi wengi zaidi walimaliza darasa la saba? | | |
| | b) | Jumla ya wanafunzi wangapi waliza daras la saba mwaka 2014 na 2015? | | |
| | c) | Mwaka upi wanafunzi wachahce zaidi walimaliza darasa la saba? | | |
| | d) | Tafuta tofauti ya idadi ya wanafunzi waliomaliza mwaka 2014 na 2017. | | |
| | e) | Je, jumla ya wanafunzi wangapi walimaliza shule katika hiyo miaka minne? | | |



Find this and other free resources at:
https://maktaba.tetea.org